K A R U C O   C O L L E G E
An Institution of the Evangelical Lutheran Church in Tanzania
Karagwe Diocese
P. O BOX 7, KARAGWE. KAGERA. TANZANIA
Email: principal@karuco.ac.tz, info@karuco.ac.

**20/05/2025**

## TANGAZO LA NAFASI ZA WAKUFUNZI

**1.0** Uongozi wa chuo cha kilimo na mifugo **KARUCO** unatangaza nafasi za kazi kwa kada ya Sayansi ya Wanyama (Science in Animal Science) na kada ya Kilimo jumuishi (Science in Agriculture General) kama ilivyoainishwa katika tangazo hili,

### 1.1 MKUFUNZI WA KILIMO JUMUISHI (SCIENCE IN AGRICULTURE GENERAL)

### 1.2 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kufundisha masomo ya fani ya Kilimo na uzalishaji;
ii. Kutayarisha mpango kazi wa mafunzo;
iii. Kupima maendeleo ya wanachuo katika nadharia na vitendo;
iv. Kutunza vifaa vya kufundishia;
v. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa chuo na jamii;
vi. Kufanya na kutoa taarifa za utafiti;
vii. Kuendesha mafunzo ya nje ya Chuo (Outreach programs); na
viii. Kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani;

### 1.2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji awe na shahada ya sayansi ya Kilimo jumuishi (**Bachelor of Science in Agriculture General)** kutoka katika vyuo au Taasisi za elimu ya juu zinazotambuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.0 MKUFUNZI WA SAYANSI YA WANYAMA (SCIENCE IN ANIMAL SCIENCE)

### 2.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kufundisha masomo ya fani ya mifugo na uzalishaji;
ii. Kutayarisha mpango kazi wa mafunzo;
iii. Kupima maendeleo ya wanachuo katika nadharia na vitendo;
iv. Kutunza vifaa vya kufundishia;
v. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa chuo na jamii;
vi. Kufanya na kutoa taarifa za utafiti;
vii. Kuendesha mafunzo ya nje ya Chuo (Outreach programs); na
viii. Kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani;

### 2.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji awe na shahada ya sayansi ya Wanyama (**Bachelor of Science in Animal Science**) kutoka katika vyuo au Taasisi za elimu ya juu zinazotambuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Maombi yatumwe kwa mkuu wa chuo kwa njia ya barua pepe**;
emmambeki.en@gmail.com au principal@karuco.ac.tz

**Muhimu**

Mwombaji aambatanishe vivuli vya wasifu na nakala ya vyeti vyake.

**Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0786 771 832 au 0689 071 070**